# DARASA LA NANE - MWAKA 2016
# SEHEMU A: KISWAHILI

**Tumia ustadi wako wa lugha kujaliza mianya**

Ukimwi utaendelea _____1 ____ watu hasa sana ____2___ ambao wamo katika ____3____ za___4___ viini hivyo. Kupenda ___5___na ___6__ ndicho ____7___ _____8_____ ya masaibu yao .Wapenda njia ___9__ mkato za kupenda _____10 ___bila kutaka kutoa _____11____. Je, Inafaa ____12____kupata ____13_____ na kesho _____14_____na kupoteza maisha yako_______15_______.

| | A | B | C | D |
|---|---|---|---|---|
| 1. | kufurahia | kulala | kuua | kuvutia |
| 2. | vijana | wazee | watoto | ajuza |
| 3. | ujana | uzee | hatari | harakati |
| 4. | kufa | kuambukiza | kutua | kutibu |
| 5. | kicheko | anasa | furaha | huzuni |
| 6. | milele | tarehe | starehe | mgeni |
| 7. | chanzo | kionyo | shida | mwanzo |
| 8. | isitoshe | kisitoshe | ijapo | cha |
| 9. | za | wa | ya | yao |
| 10. | senze | njenye | ngenge | zenze |
| 11. | josho | jasha | maisha | jasho |
| 12. | wapi | nyinyi | yeye | nini |
| 13. | laha leo | raha jana | raha leo | laha juzi |
| 14. | Usababishe viini | Upate viini | upate viini | ulete viini |
| 15. | " " | . | ! | ? |

**kutoka swali la 16-30, jibu kuambatana na maagizo.**

16. Tamatisha methali hii mfinyanzi hula ___________
    A. Gaeni
    B. Siniani
    C. Uteoni
    D. Sahanini

17. Panga vifungu hivi angaa vilete maana moja ikusudiwayo.
    i) madhali
    ii) ya kutosha na kubakisha
    (iii) una masurufu
    (iv) Utazuru meka
    A. (iv) (i) (iii) ( ii )
    B. (iii) (i) (iv) (ii)
    C. (i ) ( ii ) ( iv) (iii)
    D. (ii) ( i) (iv ) ( iii)

18. Jina jingine la kipindupindu ni ___________
    A. Kisunzi
    B. Waba
    C. Kisonono
    D. Matubwitubwi

19. Tumia kiunganishi sina la kufanya _____ kushukuru.
    A. Ingawa
    B. Hata
    C. Ila
    D. wala

20. Andika kinyume cha: Ajuza amemwajiri kapera
    A. Sahibu ameajiriwa na kapera
    B. Shaibu amemfuta mwanamwali
    C. Shaibu amefutwa na mwanamwali
    D. Shaibu ameajiriwa na mwanamali

21. Kikembe cha farasi ni nyumbu je cha njiwa cha itwa __________

A. Kisuse

B. Saraka

C. Kipura

D. Kiongwe

22 Kivumishi kipi kisichobadilika


A. Nane

B. Njema

C. Nzuri

D. Safi

23. Kwenye herufi 2 panaitwa




A. Magharibu mwa kaskazini magharibi

B. Kusini mwa kusini magharibi

C. Kusini mwa kusini magharibi

D. Magharibi mwa kaskazini magharibi

24. Kiko cha mkono ni sawa na __________

A. Kisugudi

B. Nyonga

C. Muundi

D. Kifundo

25. Mpira ambao goli lake ni duara huitwa neti boli au ____________

A. Raga

B. Jugwe

C. Kwata

D. Mpira wa pete

26. Bahati na Riziki waliagana usiku wa manane kwa kuambiana_______

A. Masalkheri

B. Aheri

C. Alamsiki

D. Binuri

27. Kumi ni kwa tita kama vile ________ ni kwa nyama.

A. Kipeto

B. mnofu

C. Topa

D. Tumbi

28. Ni sentensi ipi sahihi?

A. Mwanangu, wafanyani mama alimwuliza?"

B. " Mwanangu wafanyani?" mama alimwuliza."

C. Mwanangu, wafanyani." mama alimuliza"

D. Mwnangu wafanyani? mama alimwuliza.

29. Maneno yapi ambayo yote ni vielezi vya wakati?

A. Haraka, kistadi, ovyo, mno.

B. Mwakani, alasiri, bukrata, macheo

C. Maradufu, mfululizo, chache, tele

D. Leo, asubuhi, vuli, mwaka jana.

30. Tulifika kiambuni saa 2:45 asubuhi ni sawa na kusema tulifika.

A. Saa nane kasorobo

B. Saa nane na robo

C. saa tatu kasorobo

D. Saa nane na dakika arobaini na tano

**Soma habari ifuatayo kisha ujibu maswali 31-40.**

Mle sina hili wala lile. Maisha yangu yaligota mwamba na kusambaratika kama kwamba yalinyanyuliwa kwaa upepo wa chamchela, kwani sina. Nina wala baba mie ni msowavyele. Maisha yangu yametawaliwa na ukiwa bin kitwea nimezama kwenye lindi la jekejeke, nalilia chooni, eeh! Mungu Bwana mwenye burhaini nirehemu kabla ya mauko yaiyobisha hodi wala simile.

Toka wavyele wangu wafarakane na sayari ya tatu masiha kwangu si maisha tena bali ni mashaka.

Wallahi dunia ni rangile sijui ipo siku nitafaharika na kunafasika kuwa mlalahai, haki sijui! mie si mtu ila ni kiatu na mtu ni kitu lakini si kitu.

31. Mie sina hili wala lile maana yake ni________
    A. mchovu
    B. Mnyonge
    C. Shupavu
    D. Mchanga
32. Badala ya kusema yaligota mwamba tungesema maisha _________
    A. Yalipiga hatua
    B. Tia fora
    C. Yaligonga mwamba
    D. Yalienda joshi
33. Mtu asiye na mama wala abu_________
    A. Kiokote
    B. Mwanahalali
    C. Mwana mkembe
    D. Mwanaharamu
34. Maisha yametawaliwa na ukiwa bin kitwea maana yake ni _________
    A. Amani
    B. Upendo
    C. Furaha
    D. Upweke
35. Mwandishi alizima kwenye lindi la_________
    A. Raha
    B. Msowavyele
    C. Bashasha
    D. Majonzi
36. Wazazi kufarakana na sayari ya tatu ni________
    A. Kulilia raha
    B. Kuwakosa wavyele
    C. Kufa
    D. Kuishi katika hali ya upweke
37. Maana ya methali " dunia ni rangi rangile "ni
    A. Duia ni yenye matatizo
    B. Dunia ni badilifu sana
    C. Dunia ni ya upendo
    D. Dunia yenye amani.
38. Katika taaarifa neno mlalahai limepigwa mstali linamaanisha
    A. Mwenye mali kupindukia
    B. Mkubwa
    C. Bila unyonge
    D. Mlalahoi
39. Mbona mwandishi anajitweza?
    A. Kwa kuwa bila mzazi
    B. Kwa kuwa na upweke
    C. Kwa kuwa katika hali ya unyonge
    D. Kwa kuwa na ukiwa bini kitwea
40. mada bora kwenye habari hii ni
    A. kilio cha mnyonge
    B. Kufiwa na wazazi
    C. Maisha ya laana
    D. Maiasha ya taabu

**Soma taarifa ifutayo kisha ujibu maswali 41 - 50.**

Tunakabwa na mchachatiko wa furaha tunaposikia kiswahili kilivyopiga hatua. Ukiona vyaelea hakika vimeundwa. Kiswahili kimetoka mbali na kuwafanya wakereketwa wengi kuwa jasho katika kukikuza na kukitukuza kikiwa isirafu na ishirafu. Kiswahili kimekuwa na vikwanzo vya tata na tete. lakini wapenzi wengi wa kiswahili walifunga nira zaidi ya sana hadi kufikia pale kilipo sasa hawajachoka na hawajawahi kulaza damu kukisarifu na kukieneza.

Kabla ya kuja Istiimari, watu wengi walikipendelea lugha zao zamwanzo kuliko lugha za kuisuka pale pale kiswahili kikapenya fya! Hasa katika jamii za bara. Wale waliokipenda na kukienzi kiswahili walichukuliwa kuwa waswahili. Wakati huo njia za mawasiliano zilikuwa haba.

41. Mbona binadamu anakuwa na mchachaliko wa furaha?
   A. Jinsi tunavyokisikia kiswahili
   B. Kwa sababu kiswahili kimeendelea
   C. Kwa sababu ukiona vyaelea vimeundwa.
   D. Kiswahili kimeiga hati.

42. Ni usemi upi sawa na, ukiona vyaelea vimeundwa
   A. Haba na haba hujaza kibaba
   B. Tui ni nazi ya kwanza
   C. Siku za mwizi ni makumi mane
   D. Maji hufuata mkondo

43. Wakereketwa wa kiswahili ni kina nani?
   A. Walimu
   B. Wasomi
   C. Washabiki
   D. Waanzilishi

44. Vikwanzo vya tata na tele ni vikwanzo vya _____
   A. Matatizo na kizingiti
   B. Urahisi na kisiki
   C. Matatizo na bidii
   D. Matatizo na wepesi

45. Kuyifunga nira ni kufanyaje?
   A. Kufa moyo
   B. Kuyifunga chuma fulani
   C. Kujitahidi
   D. Kupoteza tumaini

46. Kiswahili ni lugha ya __________
   A. Watu wa bara tu
   B. Wote wanaoongezea
   C. Watu wa pwani tu
   D. Wageni

47. Istiimani ni watu wa sampuli gani?
   A. Watoro
   B. Wakoloni
   C. Walowezi
   D. Waswahili

48. Hatimaye kiswahili kilipenya fya! Hasa _______
   A. Sehemu mbali na pwani
   B. Pwani
   C. Sehemu karibu na bahari
   D. Ufukwe

49. Wakati uo huo nyenzo za mawasiliano zilikuwa
   A. Nyingi
   B. Tele
   C. Chache
   D. Sana

50. Mada ifaayo makala haya ni
   A. Kiswahili na uenesi wake
   B. Lugha za asili
   C. Wakereketwa
   D. Ukiona vyaelea vimeundwa